BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa rehma zake za kutujaalia uhai na afya njema iliyotuwezesha kukutana hapa kwa lengo la kujadili na kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Aidha, nachukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kutumia hekma na busara zako katika kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa maslahi ya wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika:** Kamati inatumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuaminiwa tena na wananchi kwa kumpa jukumu la kuingoza Zanzibar kwa kipindi cha pili. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie nguvu na ari ya kuitumikia Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika:** napenda pia, kutumia fursa hii adhimu kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza hili, kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka *2024* zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika:** aidha, niwapongeze na kuwashukuru viongozi wa Ofisi hii

wakiongozwa na Waziri hodari na mchapakazi Mheshimiwa Idrisa Kitwana Mustafa, Katibu Mkuu wake ndugu Issa Mahfoudh Haji na Afisa Mdhamini Pemba ndugu Thabit Othman Abdallah. Aidha, niwapongeze na kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makamanda wa Vikosi vya Idara Maalum za SMZ na watendaji wote wa Ofisi hii kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupatia wakati waupitiaji wa bajeti ya wizara yao.

**Mheshimiwa Spika:** kwa namna ya kipekee, nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya wajumbe wa kamati hii kwa kuonesha umahiri na ushirikiano wao mkubwa katika kutekeleza majukumu waliyopewa.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa ruhusa yako naomba sasa kuwatambulisha wajumbe wa kamati hii kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Aza Januar Joeph | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Mmanga Mohammed Hamed | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Mahfoudh Abdalla Mohammed | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Mahmoud Shineni Ali | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Masoud Amour Masoud | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *10.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| *11.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |
| *12.* | Ndg. Hassan Lila Mrisho | Afisa Bajeti |

**Mheshimiwa Spika:** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imetumia vyema nafasi yake ya kupitia, kuchambua na kuidhinisha programu zote zilizopangwa kufanyiwa kazi kwa mujibu wa Mafungu (votes)
kwa Bajeti ya Ofisi hii kama ilivyoelekezwa katika kanuni ya 119(3) Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka *2024*.

**Mheshimiwa Spika:** ni imani ya Kamati yetu kwamba kupatikana kwa fedha zilizokadiriwa kutumika katika mafungu hayo kutasaidia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa malengo ya Serikali sambamba na miradi ya kimaendeleo inayotekelezwa kwa maslahi ya nchi yetu.

**PROGRAMU ZA MAKAO MAKUU, PROGRAMU ZA SERIKALI ZA MITAA NA WAKALA WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR**:

**Mheshimiwa Spika:** kamati inaishukuru na kuipongeza Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mita ana Idara Maalum za SMZ kwa kutekelza vyema majukuu yake kwa kipindi cha mwaka uliopita kutokana na kukamilisha uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Aidha, kamati imeridhishwa na utekelezaji wa programu kuu na ndogo zilizopangwa katika mafungu ya ofisi hii ikiwemo **fungu 004** la makao makuu ambao linasimamia uongozi na utawala, usiamamizi wa Idara Maalum na uratibu wa utawala wa mikoa na serikali za mitaa.

**Mheshimiwa Spika:** sambamba na hayo, kamati inaishauri wizara kupitia progamu ya uongozi na utawala kuandaa miradi ambayo itaibua ujenzi wa majengo ya makao makuu ya wizara kwa upande wa Unguja na Pemba kutokana na uwepo wa changamoto ya uhaba wa ofisi yenye kukidhi mahitaji ya watumishi na wakati wa sasa.

**Mheshimiwa Spika:** kwa upande mwengine, kamati yetu katika upitiaji wa mapato ya fungu hili ilipata changamoto ya kutoonekana kwa mapato yaliyopangwa kutoka Hazina kwa mwaka wa fedha 2026/2027 licha ya kazi nzuri ya ukusanyaji wa mapato iliyofanywa kwa mwaka huu unaoendelea wa 2025/2026. Aidha, Kamati yetu inaipongeza wizara kwa ukusanyaji mkubwa wa mapato kupitia fungu la **D01** ambalo sasa ni **004** ambapo imeonekana ipo haja ya kuongezewa kiwango cha makadirio ya makusanyo hayo kutoka bilioni moja na milioni mia nane hadi kufikia bilioni mbili na milioni mia nne kwa mwaka huu wa fedha. Kamati inaitaka wizara kuhakikisha imesimamia vyema ukusanyaji wa mapato haya na kuona matarajio yaliyowekwa yamefikiwa.

**Mheshimiwa Spika:** kwa upande wa serikali za mitaa ambazo zinajukumu kubwa kuweka mazingira ya miji safi na salama Pamoja ukusanyaji wa mapato wenye kufuata kanuni na taratibu za ukusanyaji wa mapato katika maeneo husika. Kamati imebiani kuwepo kwa baadhi ya Mabaraza ya miji na Manispaa kukusanya mapato kwa kiwango kisichoridhisha na kupelekea kutofikia malengo yaliyopangwa katika ukusanyaji wa mapato kwa taasisi hizo. Kwa mnasaba huo, kamati inazitaka manispaa kuongeza kasi katika shughuli za usafi wa miji pamoja na kubuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitasaidia kukuza ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo hivyo.

**Mheshimiwa Spika:** Kamati inaeleza kusikitishwa kwake na kiwango kidogo cha ukusanyaji wa mapato katika Baraza la Mji Wete, hali inayotokana na kutotumika ipasavyo kwa rasilimali zilizopo, ikiwemo Soko la Wajasiriamali la Kifumbikai Wete, pamoja na kushindwa kubuni na kuanzisha vyanzo vipya vya mapato. Kutokana na hali hiyo, Kamati inazitaka taasisi za Serikali kuhakikisha zinalipa kwa wakati mgao unaostahiki kwa halmashauri, hususan katika shughuli za uchimbaji wa mchanga, kifusi na mawe, ili kuongeza mapato ya mamlaka za serikali za mitaa na kuchochea maendeleo ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika:** kadhalika, Kamati inasisitiza umuhimu kwa taasisi za umma kuwashirikisha wananchi kikamilifu katika hatua zote za kuanzisha, kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Ushirikishwaji huo utaongeza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma, sambamba na kujenga hali ya wananchi kuiona miradi hiyo kuwa ni mali yao. Vilevile, hatua hiyo itasaidia kuhakikisha miradi inayotekelezwa inaendana na mahitaji halisi ya wananchi na hivyo kuleta tija kwa jamii pamoja na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika:** kwa upande mwingine, Kamati inalipongeza Baraza la Mji Mkoani kwa kuendelea kuonyesha kiwango kizuri cha ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na matumizi mazuri ya rasilimali zilizopo katika baraza hilo. Aidha, Kamati inaridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na baraza katika kuhakikisha mazingira ya mji yanakuwa safi, salama na yenye kuvutia, hali ambayo imeendelea kuongeza hadhi ya mji huo pamoja na kuboresha ustawi wa wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika:** kama ilivyoelezwa awali, jukumu kuu la mamlaka za miji na manispaa ni kuhakikisha kuwepo kwa mazingira safi, salama na yenye kuvutia kwa wananchi pamoja na wageni wanaoingia nchini. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na hali ya usafi katika baadhi ya maeneo ya Manispaa ya Chake-Chake, hususan maeneo ya Nyumba za Maendeleo na Machomane, ambapo bado kuna changamoto zinazohitaji hatua za haraka za usimamizi na uboreshaji wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika:** kutokana na hali hiyo, Kamati inaiagiza Manispaa ya Chake-Chake kuhakikisha inatumia ipasavyo rasilimali zake katika kuimarisha huduma za usafi wa mazingira, ukusanyaji wa taka pamoja na kuweka mazingira salama kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo. Kamati inaamini kuwa utekelezaji wa hatua hizo utaongeza ustawi wa wananchi na kuimarisha taswira ya mji huo kwa wageni na wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika:** aidha, Kamati inaitaka Manispaa hiyo kufanya utafiti wa kitaalamu na wa kina kuhusu mpango wa ujenzi wa soko jipya katika eneo la Melitano, Chake-Chake. Kamati inaeleza kuwa kuna umuhimu wa kufanya tathmini ya kutosha kutokana na mzunguko mdogo wa wananchi katika eneo hilo pamoja na gharama kubwa zinazotarajiwa kutumika katika utekelezaji wa mradi huo, ili kuhakikisha uwekezaji huo unakuwa na tija ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi pamoja na Serikali.

**Mheshimiwa Spika:** Ofisi ya Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ni miongoni mwa taasisi muhimu za kijamii nchini kutokana na jukumu lake la msingi la kusimamia usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka pamoja na utoaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Kutokana na usimamizi na uendeshaji mzuri wa ofisi hiyo, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa majukumu yake, hususan kwa kufanikiwa kuanzisha ujenzi wa miundombinu ya huduma za matukio ya kijamii katika Wilaya ya Kaskazini "B" Mahonda, kuimarisha matumizi ya huduma za kidijitali pamoja na kuendelea kuhamasisha wananchi kujisajili katika matukio mbalimbali ya kijamii.

**Mheshimiwa Spika:** pamoja na mafanikio hayo, Kamati inaona bado kuna haja kubwa ya kuimarishwa kwa mazingira ya kazi na utoaji wa huduma katika Ofisi ya Wakala wa Matukio ya Kijamii. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha

Ofisi za Wilaya za Wakala huo zinapatiwa majengo mapya yenye kukidhi mahitaji ya wananchi pamoja na kuendana na matumizi ya teknolojia za kisasa. Sambamba na hilo, ipo haja ya kuzipatia ofisi hizo samani za kisasa, vifaa muhimu vya kazi pamoja na kuongeza idadi ya watumishi wenye ujuzi na uzoefu wa matumizi ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

**Mheshimiwa Spika:** vilevile, Kamati inasisitiza umuhimu kwa Wakala kuendelea kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu umuhimu wa usajili wa vyeti vya ndoa pamoja na matumizi ya huduma zinazotolewa na ofisi hiyo kwa ujumla. Hatua hiyo itasaidia wananchi kupata haki zao za msingi, kuimarisha utambuzi wa kisheria wa matukio ya kijamii na kuiwezesha Serikali kuwa na takwimu sahihi kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya taifa.

**PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU 042 – 046):**

**Mheshimiwa Spika:** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Mafungu ya Idara Maalum za SMZ **(Fungu 042 – 046)** yataendelea kutekeleza programu kuu mbali mbali ambazo zina lengo la kuweka uwiano wa Idara zote za SMZ katika masuala ya kiutawala. Kamati imeridhika na utekelezaji bora wa vikosi vyetu vya SMZ kwa kushirikiana na vikosi vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kwa kutekeleza jukumu zito la kulinda, kusimamia na kudumisha usalama wa raia na mali zao kwa msingi wa kudumisha amani na utulivu kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika:** kwa upande wa **Fungu 042** – Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), taasisi hiyo imepanga kukamilisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo mradi wa ujenzi wa dakhalia ya Skuli ya JKU Mtoni pamoja na mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wakala wa Ulinzi wa JKU. Kamati inaona kuwa utekelezaji wa miradi hiyo utasaidia kuimarisha mazingira ya kazi, kuongeza ufanisi wa utendaji pamoja na kukuza uwezo wa taasisi hiyo katika kutekeleza majukumu yake ya kiulinzi na maendeleo ya kijamii.

**Mheshimiwa Spika:** hata hivyo, pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Wakala wa Ulinzi wa JKU katika kuongeza ukusanyaji wa mapato, Kamati inasikitishwa na baadhi ya taasisi za Serikali kushindwa kulipa madeni wanayodaiwa na wakala huo

kwa wakati. Hali hiyo imekuwa ikirudisha nyuma juhudi za wakala katika kujiendesha kwa ufanisi na kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato yaliyopangwa. Kutokana na hali hiyo, Kamati inazitaka taasisi husika kuhakikisha zinalipa madeni yao kwa wakati ili kuiwezesha Wakala wa Ulinzi wa JKU kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuongeza mchango wake katika mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika:** Mheshimiwa Spika, Chuo cha Mafunzo (Fungu 043) kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kimepanga kuendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi wa chuo hicho sambamba na kuimarisha huduma za uendeshaji na utawala. Katika utekelezaji wa programu zake kwa mwaka huu wa fedha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kikosi, hususan miradi ya uzalishaji mali, ili kuiwezesha Idara hiyo kujitegemea kiuchumi na kuongeza uwezo wake wa kujiendesha kwa mafanikio zaidi.

**Mheshimiwa Spika:** kwa upande mwengine, Kamati inakipongeza kikosi hicho kwa kuendelea kusimamia vyema haki za wanafunzi pamoja na maslahi ya askari wake, jambo ambalo limekuwa msingi muhimu wa kuimarisha nidhamu, uwajibikaji na mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali pamoja na uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kunapatikana magari maalumu ya kuwahudumia wanafunzi wa chuo hicho katika shughuli zao za kila siku. Hatua hiyo itasaidia kuimarisha usalama na urahisi wa usafiri kwa wanafunzi pamoja na kupunguza hatari mbalimbali zinazoweza kujitokeza, ikiwemo matukio ya wanafunzi kutoroka au kupata madhara wanapokuwa katika mazingira yasiyo rasmi ya usafiri.

**Mheshimiwa Spika**: kwa ujumla Kamati inaridhishwa na utendaji wa Idara Maalum kutokana na mchango mkubwa wanaoutoa katika kuimarisha amani, usalama na utulivu uliopo nchini. Kutokana na umuhimu huo, Kamati inaziomba Idara hizo kuendelea kuongeza kasi ya utekelezaji wa majukumu yao, kuimarisha miundombinu ya kambi pamoja na kubuni na kusimamia miradi mikubwa ya maendeleo na uzalishaji mali itakayosaidia kuongeza mapato yao ya ndani na kuipunguzia Serikali baadhi ya gharama za uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika**: Kamati pia, inasisitiza kuwa katika kuanzisha na kutekeleza

miradi hiyo, ni muhimu kuzingatia vipaumbele vya taifa pamoja na kuwekeza katika miradi yenye tija kwa vikosi husika na jamii inayowazunguka, ili miradi hiyo iweze kutoa manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa muda mrefu.

HITIMISHO:

**Mheshimiwa Spika:** naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya kamati yangu na niwashukuru pia, Makamanda wa Idara Maalum za SMZ, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi, Madiwani, Masheha na watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa utendaji wao na uzalendo wao na mashirikiano yao katika kutekeleza majukumu ya Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika:** mwisho, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wairidhie, waichangie na waipitishie mapato ya **shilingi 8,799,956,000/-** kuchangia mfuko mkuu za serikali na kuidhinisha mapato ya ndani ya **shilingi 25,995,938,400/-** yatakayokusanywa na kutumiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, kamati inaliomba baraza lako tukufu kujadili na kuidhinisha matumizi ya **shilingi 732,967,770,000/-** kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika:** kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa *Naunga Mkono Hoja.*

Ahsante;

.......................................

(Mhe. Machano Othman Said)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR